

**OFISI YA RAISI – TAWALA ZA MIKOA NA SELIKARI ZA MITAA.**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA.**

**MAAGIZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA 2021.**

SHULE YA SEKONDARI  
KAYAO,  
S. L. P. 371,  
**NJOMBE.**  
05/ 12/ 2020.

Ndugu; \_\_\_\_\_  
S. L. P. 19, LUDEWA,  
\_\_\_\_\_.

**A. UTANGULIZI.**

Awali ya yote nipande kukupongeza kwa kachaguliwa kujiunga kidato cha **kwanza** shule ya sekondari **Kayao** kwa mwaka **2021**.

**B. MAZINGIRA YA SHULE.**

Shule ya sekondari Kayao ipo katika kijiji cha Mangalanyene, kata ya Madope, wilaya ya Ludewa na mkoa wa Njombe. Shule ipo umbali wa kilomita 7 toka barabara kuu ya Njombe – Ludewa toka kijiji cha Madope (LUSITU).

**C. MAAGIZO MBALIMBALI.**

Shule itafunguliwa mnamo tarehe **11/ 01/ 2021**

**I. MAAGIZO YA SHULE.**

**WAVULANA.**

Mwanafunzi aje na mahitaji yafuatayo kwaajili ya matumizi yake binafsi:

1. Suluari mbili rangi ya damu ya mzee.
2. Mashati MAWILI meupe mikono mirefu.
3. Sweta la **V** rangi ya **blue**.
4. Suluari 2 rangi nyeusi.
5. Tisheti 2, (rangi ya Bluu 1, na rangi nyekundu 1)
6. Viatu vya kamba juzi 2( **sio raba**)
7. Soksi rangi nyeusi.
8. Godoro la futi  $2\frac{1}{2} \times 6$
9. Shuka rangi ya Laiti bluu, blanketi zito, na mto.
10. Vifaa vya michezo ( viatu vya michezo, bukta nyekundi au kijani, fulana ya michezo nyekundi au kijani na soksi za michezo)
11. Track suti rangi nyeusi.

### **WASICHANNA.**

Mwanafunzi aje na mahitaji yafuatayo kwaajili ya matumizi yake binafsi:

1. Suluari mbili rangi ya damu ya mzee.
2. Kisoro cha kuishia kwenye magoti kata mikono rangi ya damu ya mzee (**kitambaa cha suluari**).
3. Mashati MAWILI meupe mikono mirefu.
4. Sweta la **V** rangi ya bluu.
5. Gauni rangi ya damu ya mzee la kuvala baada ya masomo.
6. Traki suti rangi ya laiti bluu.
7. Viatu vyeusi vya ngozi vya kamba, jazi 2, sio raba.
8. Soksi zaidi ya jazi 2 rangi nyeupe.
9. Shuka rangi ya pinki, blanketi zito na mto
10. Godoro la futi  $2\frac{1}{2} \times 6$ .
11. Tisheti 2 (bluu 1 na nyekundu 1)
12. Raba za michezo.

### **MAHITAJI MUHIMU KWA WOTE.**

1. Ndoo ya kuogea,
2. Taulo au kanga/kitenge kipande 1 kwa wasichana.
3. Madaftari makubwa 12 ( counter books)
4. Mkebe wa hesabu na kalamu za kutosha.
5. Nguo za ndani za kutosha. (**zitakaguliwa**)
6. Sabuni, dawa ya mswaki, mswaki, kiwi na brashi zake,
7. Na mahitaji mengine muhimu kwa mtoto husika.

### **II. MAAGIZO YA KAMMATI YA WAZAZI.**

Kila mwanafunzi atachangia michango ifuatayo:

### **CHAKULA**

1. Mahindi dene 12 kwa mwaka. ( yatolewe awamu 1)
2. Maharage dene 3 kwa mwaka, yatolewe awamu ya kwanza debe 2 na muhula wa pili debe 1.
3. Fedha kiasi cha shilingi 165,000/= itolewe awamu 2, awamu ya kwanza 100,000/= na muhula wa pili 65,000/=

### **MAHITAJI MENGINE.**

1. Bunda moja la karatasi **A4**
2. Kindoo kidogo cha lita 10 kwaajili ya kuendeshea shughuli za chakula.